

TANZANIA LOCAL GOVERNMENT REFORMS ASSOCIATION



Kumb. Na TOA/C.1/01/98

19 Julai, 2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

TOA (Tanzania Local Government Reforms Association) ni Taasisi inayohusika na maboresho katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi (D by D). Aidha TOA inahamasisha usimamizi na uboreshaji wa utoaji huduma za jamii (Afya, Elimu, Kilimo, Biashara, Miundo Mbinu na Maji) Usimamizi wa Rasilimali Watu, Fedha, Miradi ya Maendeleo pamoja na Utawala Bora. Taasisi hii inaundwa na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara pamoja na wanachama wengine waliopo nje ya OR - TAMISEMI

Katibu Mkuu wa TOA anatangaza nafasi ya kazi ya Afisa wa Miradi, atakayefanya kazi na Taasisi ya TOA Mkoani Dodoma. Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi hii wanakaribishwa kuomba kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.

1. AFISA MRADI (PROJECT OFFICER) - NAFASI 1

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- Kuajiriwa mwenye Shahada/Stashahada ya juu katika fani ya Uchumi, Usimamizi wa Miradi, Mipango ya Uwekezaji na Maendeleo ya Fedha kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- Mwenye uzoefu usiopungua miaka mitatu.

B. KAZI NA MAJUKUMU YA MRATIBU WA MIRADI

- Kubuni, kuandika na kusimamia miradi ya taasisi.
- Kufanya ufuatiliaji wa miradi
- Kubuni mbinu zitakazosaidia kuongeza faida katika miradi
- Kuandaa na kuratibu mikutano na wadau wa Taasisi
- Kumshauri Katibu Mkuu kuhusiana na mienendo ya mradi.
- Kushauri juu ya udhibiti wa viatarishi vya miradi (Risk Management)

C. MSHAHARA

Kulingana Na viwango vya mshahara wa TOA

D. ENEO LA KAZI - Makao Makuu ya TOA yaliyopo Jiji la Dodoma

E. MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenyewe umri usiozidi miaka 45.
- Muombaji aambatanishe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV), anwani na namba za simu za mkononi.
- Maombi yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na mwanasheria.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **1/8/2022** saa tisa na nusu jioni.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'J. M. M.', is enclosed in a blue oval. Below the oval, the text 'KATIBU MKUU' and 'TOA' is printed in capital letters.

Maombi yote yatumwe kwa: -

**KATIBU MKUU WA TOA
S. L. P. 1923
DODOMA**